

Hati ya msaada wa dharura kwa watu walioathiriwa na tatizo la magonjwa ya COVID-19 – toleo la mji wa Charlottesville pamoja na wilaya ya Albemarle

**Tafsiri ya 3, imesasishwa tarehe 15/5/2020**

*Hati hii inatoa orodha ya msaada wa eneo letu, imesasishwa ili kufuata hali ya kisasa wakati wa tatizo la COVID. Nambari zote za simu ni za simu ya eneo 1-434 isipokuwa kama imeandikwa nambari nyingine. Kwa habari kamili za kisasa elekeza kamera ya simu ya mkononi kwenye “QR code” hapo chini ambayo itakuonyesha ukurasa wa intaneti.*

**CHAKULA CHA UMMA**

- The Haven; anwani 112 W Market Street; unaweza kufika kwa kutembea
- Salvation Army; anwani 207 Ridge Street; unaweza kufika kwa kutembea
- Keevil & Keevil Kitchen; anwani 703 Hinton Ave; uwatumie barua pepe keevilkitchen@gmail.com au upige simu ya 989-8807.

	Chakula cha asubuhi	Chakula cha mchana	Chakula cha jioni
The Haven	Jumatatu-Jumapili (saa moja asubuhi)	Jumatatu-Alhamisi (saa sita mpaka saa saba mchana)	
Salvation Army	Jumatatu-Jumamosi (saa moja asubuhi)  Jumapili (saa tatu asubuhi)	Ijumaa-Jumamosi (saa sita mchana)  Jumapili (saa saba mchana)	Jumatatu-Jumamosi (saa kumi na moja na nusu jioni)
Keevil & Keevil	Jumatatu-Ijumaa (saa mbili asubuhi)	Jumatatu-Ijumaa (saa sita mchana)	

## MALAZI YA DHARURA

- **Salvation Army Emergency Shelter:** simu 295-4058; anwani 207 Ridge St. Kwa wanaume, wanawake, familia, watoto. Piga simu au ufike saa nne asubuhi hadi saa nne jioni – *kwa sasa hawapokei wageni wapya.*
- **PACEM:** (simu ya Liz) 465-1391; anwani 112 W Market St (ofisi) – wanawapokea wageni wapya lakini si wengi, utahitaji kumpigia simu Liz ili kuhakikisha kama kuna nafasi.
- **Shelter for Help in Emergency (SHE):** Piga simu ya “hotline”: 293-8509. Makazi kwa waathiriwa na ujeuri wa nyumbani. Wanawapokea wageni wapya, piga simu ya “hotline”.
- **ReadyKids-Runaway Emergency Services (ReadyKids-Msaada kwa Watoto Waliotoroka Nyumbani) :** Piga simu ya “hotline” 972-7233; kazi yake inaendelea.
- **Families in Crisis (Familia Zilizo na Shida Kubwa):** Simu 296-3872. *Kwa sasa, pesa za kuwasaidia watu kupata malazi zimekwisha;* bado unaweza kupiga simu kwa mashauri mengine.

## Idara ya Huduma za Jamii

Ili kuomba msaada wa Medicaid, SNAP, TANF, na manufaa mengine

- Simu 1-855-635-4370 ama uende kwenye intaneti ili kuomba msaada
- Piga simu ya 1-855-242-8282 ili kuomba msaada wa Medicaid

Kwa mahitaji mengine, piga simu ya 970-3400 (Charlottesville) au 972-4010 (Albemarle). Ofisi zenyewe zimefungwa kwa umma.

## Msaada wa Kujua Kusoma na Kuandika / GED

- **Thomas Jefferson Adult Career Education (TJACE):** Simu 961-5461. Kujitayarisha kwa digrii ya GED, kujua kusoma na kuandika, kujitayarisha kwa kazi mbalimbali. Mafunzo yanaongozwa kwenye intaneti tu, upige simu na kuacha ujumbe ili kupata habari zaidi.
- **Literacy Volunteers of America:** simu 977-3838; anwani 233 4<sup>th</sup> St NW (Shule ya Jefferson). Msaada wa kujua kusoma na kuandika, msaada wa kujifunza Kiingereza. *Kwa sasa ofisi hii imefungwa.*

## Msaada kwa Wanajeshi Waliostaafu

- **VA Medical Center (Mahali pa Matibabu kwa Wanajeshi Waliostaafu):** Simu 293-3890; anwani 590 Peter Jefferson Pkwy #250. Aina zote za msaada na masaa ya kufunguliwa hayakubadilika.

- **Supportive Services for Veteran Families (Msaada kwa Familia za Wanajeshi Waliostaafu):** Simu 804-788-6825. Huduma za haraka za kuwasaidia watu kutafuta malazi na misaada mingine. Ofisi imefungwa, piga simu ili kuomba msaada.

- **Virginia Department of Veterans Services (Idara ya Huduma kwa Wanajeshi Waliostaafu ya Jimbo la Virginia):** simu 804-691-4905; anwani 1430 Rolkin Ct, Chumba 202. Uchunguzi kwa msaada wa wanajeshi waliostaafu, mashauri, afya ya akili, malazi. Ofisi imefungwa, piga simu ili kupata habari.

## **MSAADA KWA WATU WALIOPOTEZA KAZI**

- **Virginia Employment Commission (Tume ya Kazi ya Virginia):** simu 1-866-832-2363. Piga simu au utumie intaneti ili kuomba msaada huo.

- **Goodwill Industries of the Valley:** simu 1-540-581-0620. Mafunzo ya bure ya kazi mbalimbali na mashauri kuhusu shughuli yanaongozwa kwenye intaneti.

- *Ofisi zifuatazo zimefungwa:* Downtown Job Center, Network2Work. Virginia Workforce Center pia imefungwa.

## **NGUO**

- **Duka la Salvation Army Thrift Store:** simu 979-5320; anwani 605 Cherry Ave. Bado liko wazi.

- **Eden Ministries:** Nguo na vyombo vya nyumbani vya bure. Kwa habari zaidi tazama hapo chini "Chakula cha Dharura". Iko wazi.

- **THRIVE Women's Health:** Nguo kwa wanawake wenye mimba. Simu 220-3777, anwani 1416 Greenbrier Pl. Upige simu kabla ya kufika.

- *Maduka ambayo yamefungwa kwa sasa:* Green Olive Tree (Crozet), Belmont Baptist Clothing Closet, Twice is Nice

## **USAFIRISHAJI**

- **JAUNT:** simu 296-3184. Usafirishaji wa eneo hili.

- **City of Promise:** simu 288-5153. Lifti za bure za Lyft kwa wakaaji wa Hardy Dr, 10<sup>th</sup> na Page, na Starr Hill

- **Baisikeli za Veo E-bikes:** simu 1-855-VEO-2256. Matumizi ya bure ya e-bike *mpaka mwisho wa mwezi wa Mei*. Pakua app ya Veo au piga simu ili kufungua akaunti na kutumia baisikeli.

## HUDUMA ZA KUPINGA UBAGUZI

- **Legal Aid Justice Center (Kituo cha Msaada wa Kisheria na cha Haki):** simu 977-0553; anwani 1000 Preston Ave #A. Mashauri ya kisheria kuhusu ubaguzi wa malazi na wa kazi, haki za raia, uhamiaji. Ofisi imefungwa, piga simu ili kuomba msaada.
- **Central Virginia Legal Aid Society (Shirika la Msaada wa Kisheria la Virginia ya Kati):** simu 296-8851; anwani 1010 Preston Ave. Mashauri ya kisheria kuhusu kufukuzwa nyumbani, kuchukuliwa kwa mali ya mkopaji aliyeshindwa kulipa, ujeuri wa nyumbani. Hawapokei watu wanaofika tu, wapigie simu au uende intaneti ili kuomba msaada.
- **Office of Human Rights (Ofisi ya Haki za Binadamu):** simu 218-0756; anwani 106 5<sup>th</sup> St NE. Utetezi, usuluhisho, na upelelezi wa ubaguzi wa malazi, kazi, na manufaa. Ofisi imefungwa, piga simu ili kuomba msaada.

## MSAADA MWINGINE WA DHARURA

- **AIM:** simu 972-1704. Jumatatu-Alhamisi kutoka saa tatu asubuhi mpaka saa kumi jioni. Msaada wa malipo ya gharama za matumizi na za malazi. Piga simu kwa Salvation Army kwa msaada wa gharama za umeme au kupashajoto, kwa mambo mengine uende intaneti.
- **Love INC:** simu 977-7777. Msaada wa dharura wa kifedha na wa aina nyingine. Ofisi imefungwa, piga simu ili kuomba msaada.
- *(Kwa wakaazi wa Kaunti ya Albemarle tu):* **Kanisa la Crozet Baptist Church:** simu 973-4281. Ili kupata taarifa kuhusu misaada ya eneo letu.
- **Community Emergency Response Fund:** *Imefungwa. Haipokei maombi tena.*

## UNAHITAJI HABARI ZAIDI? Elekeza kamera ya simu ya mkononi kwenye QR code hii hapa

ili kufungua ukurasa wa intaneti wenye maarifa ya kisasa juu ya misaada iliyotajwa katika hati hii, ama uende hapa: <https://tinyurl.com/covidresourceguidecville>

SCAN ME

## AFYA YA WANAWAKE NA WASICHANA

- **Charlottesville Health Center – Planned Parenthood:** simu 296-1000; anwani 2964 Hydraulic Rd. Huduma za utoaji mimba, udhibiti wa uzazi, kupimwa kwa ukimwi, kupata dawa za dharura za kuzuia mimba, kupimwa na kutibiwa kwa magonjwa yanayoambukizwa kingono, kupimwa mimba na misaada mingine. Iko wazi.
- **Whole Woman’s Health:** simu 973-4888; anwani 2321 Commonwealth Dr. Huduma za utoaji mimba, udhibiti wa uzazi, kupimwa kwa ukimwi, kupata dawa za dharura za kuzuia mimba, kupimwa na kutibiwa kwa magonjwa yanayoambukizwa kingono, kupimwa mimba na misaada mingine. Iko wazi.
- **Blue Ridge Abortion Fund (Hazina ya Blue Ridge ya Utoaji Mimba):** simu 963-0669. Msaada wa kifedha kwa wenye mimba wanaohitaji kutoa mimba lakini hawana pesa za kutosha.
- **Donor Diapers (Nepi za Bure):** simu 214-0345; Garrett Community Center (418 E Garrett St SE). Wanatoa nepi na vitambaa vya kupangusa mtoto (wipes) siku moja kwa mwezi. Siku ijayo ni 21 Juni, kutoka saa nane mpaka saa tisa na nusu mchana.

## MSAADA WA AFYA YA KIMWILI

- **UVA Community Call Line (Simu ya Jamii ya Chuo Kikuu cha UVA):** simu 98-COVID (982-6843, chagua namba 3); Jumatatu-Ijumaa kutoka saa mbili asubuhi mpaka saa kumi na moja jioni. Kituo kipya cha simu, wanawasaidia watu ambao hawana daktari wa kawaida kuongea na daktari wa UVA ili kuzungumzia mahitaji ya kitiba yasiyo ya dharura (kwa mfano dalili mpya, matibabu ya magonjwa ya kudumu, maagizo ya dawa).
- **Thomas Jefferson Health Department (Idara ya Afya ya Thomas Jefferson):** simu 972-6269; anwani 1138 Rose Hill Dr. Kwa sasa wanafanya uchunguzi wa pap smear na kuwasaidia watu kupata udhibiti wa uzazi tu, hawafanyi machunguzi mengine wala kutoa dawa za kuchanjia. WIC bado inafanya kazi. Lazima uwe na miadi (huwezi kufika tu). Kwa maarifa ya COVID: piga simu ya 972-6261.
- **Charlottesville Free Clinic (Kliniki ya Bure ya Charlottesville):** simu 296-5525; anwani 1138 Rose Hill Dr. Matibabu yasiyo ya kidharura na duka la madawa kwa familia zenye kipato cha chini. Matibabu ya kwenye intaneti tu, piga simu ili kuhakikisha kuwa unastahiki. Matibabu ya meno: mahitaji ya dharura tu, wagonjwa hutibiwa kwa mfuatano walivyofika.
- **Central Virginia Health Services (Neighborhood Family Health, Huduma za Afya za Virginia ya Kati):** simu 227-5264; anwani 901 Preston Ave, chumba 301. Matibabu ya

kimwili, ya meno, na ya kitabia na duka la madawa. Ada zinategemea kipato. Bado iko wazi, panga miadi kwenye intaneti.

- **Visionworks:** simu 293-3225, anwani Barracks Shopping Center. Uchunguzi wa macho wa bure kwa watu wenye Medicaid. Iko wazi.
- **MyEyeDr:** simu 973-5361, anwani 441 Westfield Rd. Mahali hapa tu: uchunguzi wa macho wa bure ukiwa na bima ya Premier, Aetna Better Health, ama MARCH Vision Medicaid. Kwa sasa: miadi muhimu tu; hivi karibuni itafunguliwa kwa uchunguzi wa macho wa kawaida.
- **Cville Community Cares:** simu 214-0454; Upelekaji wa dawa nyumbani wa bure. Uende <http://tinyurl.com/cvillecaresrx>
- **UVA:** Kliniki za kutolazwa sasa zinapanga mikutano ya uso kwa uso ama kwenye intaneti.

## MSAADA WA AFYA YA AKILI

- **Region 10:** Huduma za afya ya akili, ulemavu wa akili, uraibu wa dawa za kulevya. Baadhi ya huduma zinaongozwa kwenye intaneti, upige simu ili upate habari. Simu ya dharura: 972-1800 ama 1-866-694-1605. Kwa miadi za matibabu ya intaneti piga simu ya 972-1829.
- **On Our Own:** simu 979-2440; anwani 123 4<sup>th</sup> St NW. Msaada wa kirika wa afya ya akili na wa uraibu wa dawa za kulevya. Jengo limefungwa, lakini mikutano ya kuunga mkono yanaendelea kwenye intaneti.
- **Teen Crisis Hotline (Simu ya Dharura kwa Vijana):** 972-7233. Msaada kwa vijana wa umri wa miaka 12-18. Ofisi imefungwa, simu ya “hotline” bado inafanya kazi, piga simu ya “hotline” ili kupanga mkutano kwenye intaneti.
- **Women’s Initiative (Ari ya Wanawake):** simu 872-0047. Msaada na mashauri kwa wanawake na wanawake waliobadisha jinsia zao. Kliniki ya simu ya bure ipo, uende kwenye ukurasa wa intaneti ili kujua saa zake za kazi.
- **Mental Health Association Virginia Warm Line (Simu ya Shirika la Afya ya Akili la Virginia):** 866-400-6428. Msaada wa kirika kwa watu walio na taabu ama kwa wenzao wanaohangaika juu yao.
- **Grief Share (Shiriki Katika Huzuni):** simu 800-395-5755. Kikundi cha watu wanosaidiana kuvumilia huzuni ya kifo kwenye intaneti. Uende ukurasa wake wa intaneti ama upige simu.

- **Partner for Mental Health:** simu 977-4673. *Kwa sasa haifanyi kazi.*

## **MATIBABU YA URAIBU WA DAWA ZA KULEVYA**

- **Addiction Allies (Rafiki za Waraibu):** simu 260-3042. Kliniki ya dawa ya suboxone / matibabu ya dawa, mashauri juu ya uraibu na afya ya akili kwenye intaneti. Wanapokea Medicaid. Huhitaji agizo la daktari, upige simu tu au uende ukurasa wao.
- **Addiction Recovery Systems - Pantops:** simu 220-0080. Anwani 103 S. Pantops Dr. Matibabu ya methadone na suboxone, mashauri kwenye intaneti. Wanapokea Medicaid na Medicare. Huhitaji agizo la daktari. Upige simu kwa uchunguzi wa kuanzia.
- **Region 10:** Tz hapo juu, “Msaada wa Afya ya Akili”
- **Msaada wa kirika kwa uraibu kwenye intaneti,** ratibu ziko kwenye kurasa zifuatazo: **SMART Recovery, Alcoholics Anonymous** (simu 293-6565), **Narcotics Anonymous** (simu 800-777-1515), **Al-Anon** (cvillealanon@gmail.com, simu ya “hotline” 972-7011), **Al-Ateen** (senglot12@gmail.com, simu ya “hotline” 972-7011), **In the Rooms**

## **UTETEZI WA WALIOSHAMBULIWA KINGONO**

- **Shelter for Help in Emergency (SHE):** Tz hapo juu, “Malazi ya Dharura”.
- **Sexual Assault Resource Agency (SARA):** Simu ya ofisi: 295-7273; simu ya “hotline”: 977-7273. Anwani 335 Greenbrier Dr. Huduma za kuwasaidia watu walioshambuliwa kingono na kwa wenzao. Huwezi kufika ofisini; mashauri ya video na simu ya “hotline” bado vinafanya kazi.

## **CHAKULA CHA DHARURA**

- **Emergency Food Network (Mtandao wa Chakula cha Dharura):** simu 979-9180; anwani 900 Harris St. Chakula cha siku tatu, mara moja kwa mwezi. Upige simu tangu saa tatu asubuhi mpaka saa sita mchana, Jumatatu mpaka Ijumaa ili kukiomba, halafu ufike kukipata tangu saa moja na nusu mpaka saa tisa na nusu mchana.
- **Loaves and Fishes:** simu 996-7868; anwani 2050 Lambs Road. Chakula cha siku saba, mara mbili kwa mwezi. Upige simu ili kukiomba. Kukichukua kwa gari Jumatano (saa nane mchana mpaka saa kumi), Alhamisi (saa kumi na mbili na nusu mpaka saa mbili na nusu jioni), na Jumamosi (saa nne asubuhi mpaka saa sita mchana).
- *Kwa wakaaji wa Kaunti ya Albemarle tu:* **B.F. Yancey Community Center:** anwani 7625 Porters Rd, Esmont, VA. Kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi, saa kumi na moja mpaka saa moja jioni. Ufike kwa gari, hunitaji kupiga simu kabla ya kufika.

- **The Catering Outfit Helps:** Ghala ya chakula ya muda mfupi kwa wafanyakazi wa mikahawa ambao wamepoteza kazi. Jumatatu na Alhamisi kutoka saa tano mpaka saa nane mchana, uende kupata chakula kwenye Atrium karibu na njia ya Carlton Road, Charlottesville.

#### ***Makanisa yanayotoa Chakula cha Bure:***

- **Church of the Incarnation:** simu 465-2671; anwani 1465 Incarnation Dr. Jumapili tangu saa saba na nusu mchana mpaka saa kumi. Huhitaji kuomba kabla ya kufika.
- **Holy Comforter Catholic Church:** anwani 208 E Jefferson St. Jumatatu mpaka Jumatano, kutoka saa nne asubuhi mpaka saa sita mchana. Ufike tu.
- **Church of our Saviour Episcopal:** anwani 1165 Rio Rd E. Jumatatu na Jumatano saa sita na nusu mpaka saa nane mchana, Ijumaa kutoka saa nne na nusu asubuhi mpaka saa sita mchana. Liko wazi.
- **Ministerios Profeticos Palabra:** simu 1-804-216-0399; anwani 1827A Seminole Trail
- **St. Paul's Episcopal Church:** anwani 851 Owensville Rd. Kila Jumatano wa tatu kwa mwezi. Kwa wakaaji wa Albemarle ya Magharibi tu. Liko wazi; upige simu ya 979-4490 ili kuomba.
- **Thomas Jefferson Memorial Church:** anwani 717 Rugby Rd. Kila Ijumaa ya kwanza kwa mwezi, kutoka saa tatu mpaka saa tano asubuhi (ujiandikishe kabla ya saa nne asubuhi). Liko wazi, upige simu ya 293-8179 ili kuomba.
- **New Beginnings Christian Community:** anwani 1130 E Market St. Jumatano alasiri na Jumamosi asubuhi. Liko wazi, upige simu ya 249-5691 ili kuomba.
- **Bethany Seventh Day Adventist:** anwani 401 Harris Rd. Kila Jumamosi ya tatu kwa mwezi, kutoka saa saba mpaka saa nane na nusu mchana. Uandike ujumbe mfupi au upige simu ya 904-553-5167 wiki moja kabla ya kuja; watakupelekea (katika mji wa Charlottesville tu) au ufike kwa gari.
- **Eden Ministries:** anwani 2999 Merrie Meadows Lane, Keswick. Jumamosi ya kwanza kila mwezi kutoka saa tatu asubuhi mpaka saa sita. Upige simu ya 973-4068 ili kupanga saa nyingine.

#### ***Huduma za Upelekaji wa Chakula Nyumbani:***

- **Social Distance Delivery:** Upelekaji wa bure wa chakula. Uombe msaada huo kwenye ukurasa wa [socialdistancedelivery.org](http://socialdistancedelivery.org)



- **JABA Home Delivered Meals (Upelekaji wa Mlo Uliopikwa wa JABA):** simu 817-5253. Kwa watu wa umri wa zaidi ya miaka 60 na wenye kipato cha chini, ambao hawawezi kujipikia chakula wenyewe. Upige simu ili kuhakikisha kama unastahiki.

- **Meals on Wheels:** simu 293-4364. Upelekaji wa chakula cha mchana cha wiki mbili kwa watu wasioweza kutoka nyumbani. Hukipeleka mara mbili kwa mwezi. Upige simu au uombe msaada huo kwenye intaneti.

***Mlo Kwa Watoto:***

- Kaunti ya Albemarle na Mji wa Charlottesville vinatoa chakula cha asubuhi na cha mchana kwa mtoto yeyote wa umri chini ya miaka 18. Mpaka tarehe 5 Juni. Uende kurasa za intaneti ili kujua mahali na ratiba za kukichukua.